



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HWC/L.20/03/VOL/VIII/92

12.11.2024

**MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.**

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA ARDHI KWA MWEKEZAJI SUKI FOOD
COMPANY LTD WA KIJIKI CHA KWAZOKA HALMASHAURI YA CHALINZE**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Tunapenda kukutaarifu kuwa Ofisi ilipokea barua kutoka kwa Mtendaji wa kijiji cha Kwazoka akiitambulisha kampuni tajwa hapo juu ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kijiji chao ambapo kijiji kilipokea maombi ya kumilikishwa eneo lenye ukubwa wa ekari 3.4 ambazo wamenunua kutoka kwa wamiliki 3 (Kumkalile Manzo, Ester Simba na Rajabu Juma Rajabu amba oni wamiliki wa awali.
3. Mtendaji wa Kijiji alieleza kuwa Kampuni ya **SUKI FOOD COMPANY LTD** ya **DAR ES SALAAM**, hapa nikiirejea kama Kampuni ya kigeni ambayo inaomba kumilikisha shamba lenye ukubwa wa ekari tatu nukta nne (3.4) kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha vyakula mbalimbali (**Candy, Biscuits and Milk powder**).
4. Kampuni ya **SUKI FOOD COMPANY LTD** ilipata eneo hilo kutoka kwa wananchi wa kijiji cha Kwazoka. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

5. Halmashauri ya Wilaya ilipokea maombi ya kupimiwa na kumilikishwa ardhi hiyo tarehe 25/10/2024 kutoka kwa mwekezaji **SUKI FOOD COMPANY LTD** kwa mujibu wa Sheria. Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 07/11/2024 na kubaini yafuatayo:

(a) Uwepo wa eneo lenye ukubwa wa ekeri **3.4**

(b) Eneo hilo halijafanyiwa maendeleo yoyote na hakuna mgogoro wowote.

6. Kwa sababu hizo, wakati Halmashauri inaendelea na zoezi la upimaji tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ya Kampuni **SUKI FOOD COMPANY LTD** ambayo imenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wenye jumla ya ekari tatu nukta nne (3.4), Aidha, tunadhibitisha kuwa eneo hilo halina mgogoro wowote uliobainika wakati wa ukakaguzi.

7. Pamoja na barua hii, nimeambatisha Mikataba ya manunuzi, Mihtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria.

8. Naomba kuwasilisha kwa hatua zinazofuata.



Ramadhani Possi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE.



Nakala:

SUKI FOOD COMPANY LTD
P.O. BOX 25500 DAR ES SALAAM,
TANZANIA.